MFUKO WA
ELIMU
Jarida la Tisa la Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)

www.tea.or.tz | Januari - Machi | 2026



USHIRIKIANO WA TEA NA UNICEF WAINUA UFAULU WA SAYANSI SHULE ZA SEKONDARI

- MIRADI YA TEA MBULU YAINUA ELIMU KWA WATOTO KUTOKA MAZINGIRA MAGUMU UK. 6
- BWENI LA WASICHANA KICHEMA – SUMBAWANGA KUNUFAISHA WANAFUNZI 80 UK. 8

"Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu Ya Elimu"

KUHUSU TEA

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ni Taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge ya Mfuko wa Elimu Na. 8 ya 2001 chini ya kifungu cha 5 (1) ili kuratibu na kusimamia Mfuko wa Elimu, ulioanzishwa kwa sheria hiyo hiyo. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2013.

Madhumuni ya Mfuko wa Elimu ni kuongeza nguvu za Serikali katika kugharimia miradi ya elimu ili kuinua ubora wa elimu na upatikanaji wake kwa usawa, katika ngazi zote za Elimu kwa Tanzania Bara na Elimu ya Juu kwa Tanzania Zanzibar.



DIRA

Kuwa Mfuko wa Elimu bora wenye hadhi ya kimataifa unao tatua changamoto za elimu nchini, kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato katika kuchangia maendeleo endelevu nchini.



DHAMIRA

Kutafuta rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya Mfuko wa Elimu na kuzigawa rasilimali hizo kwa ufanisi katika kufadhili miradi ya elimu ili kuboresha upatikanaji wa elimu bora na ujuzi kwa usawa.

YALIYOMO

SALAAM ZA MKURUGENZI MKUU.....iii

USHIRIKIANO WA TEA NA UNICEF WAINUA UFAULU WA SAYANSI SHULE ZA SEKONDARI.....01

TEA YATOA REKODI: MIRADI 1,711 YATEKELEZWA THAMANI YA SH. BILIONI 128.5.....03

HABARI KATIKA PICHA.....04

MIRADI YA TEA MBULU YAINUA ELIMU KWA WATOTO KUTOKA MAZINGIRA MAGUMU.....06

NMB BANK YAZIDISHA FURAHA SHULENI – WANAFUNZI WENYE ULEMAVU WAFURAHI 07

BWENI LA WASICHANA KICHEMA – SUMBAWANGA KUNUFAISHA WANAFUNZI 80 08

TIMU YA UHARIRI

Mwenyekiti: Masozi Nyirenda

Mhariri: Bestina Magutu

Wachangiaji: Eliafile Solla

Joyce Minja

ANUANI:

Mamlaka ya Elimu Tanzania(TEA)

S. L.P 2516, Dodoma- Tanzania

Barua pepe: info@tea.or.tz,

Tovuti www.tea.or.tz,

Instagram: Officialteatz,

SALAMU ZA MKURUGENZI MKUU



Ndugu wasomaji,

Ni furaha kuwakaribisha katika Toleo la Tisa la Jarida la Mfuko wa Elimu, linaloangazia shughuli na mafanikio yaliyotekelezwa katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2025/2026, kuanzia Januari hadi Machi.

Katika kipindi hiki, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya elimu kwa kushirikiana na Serikali, washirika wa maendeleo, sekta binafsi na wadau wengine. Miradi hiyo imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kupitia ujenzi na ukarabati wa maabara za sayansi, mabweni, madarasa na miundombinu mingine muhimu ya elimu.

Jarida hili linaonesha mafanikio ya ushirikiano wetu na wadau mbalimbali katika kuimarisha elimu ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM), kuboresha elimu jumuishi na kuendelea kuwekeza katika maendeleo ya sekta ya elimu kwa manufaa ya watoto wa Kitanzania.

Napenda kuishukuru Serikali, washirika wa maendeleo, wadau na wananchi wote wanaoendelea kuunga mkono Mfuko wa Elimu. Ushirikiano wenu unaendelea kuwa chachu ya mafanikio tunayoyaona leo. Ninawaalika msome toleo hili na kujionea hatua mbalimbali zinazochukuliwa na TEA katika kuchangia maendeleo ya elimu nchini.

Dkt. Erasmus F. Kipesha
Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)

1. MAPINDUZI YA STEM: USHIRIKIANO WA TEA NA UNICEF WAINUA UFAULU WA SAYANSI SHULE ZA SEKONDARI

Katika kipindi hiki ambacho dunia inaongozwa na mapinduzi ya sayansi na teknolojia, uwekezaji katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) ni nguzo muhimu ya maendeleo ya taifa. Kwa kulitambua hilo, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), chini ya ufadhili wa Serikali ya Canada wamekuwa wakitekeleza miradi ya pamoja ya kuimarisha miundombinu ya maabara za sayansi katika shule za sekondari mikoa ya Kigoma, Songwe na Tabora.

Miradi hiyo imetekelezwa katika awamu mbili kuanzia Mwaka wa Fedha 2023/2024 ambapo katika awamu ya kwanza jumla ya Sh. milioni 344,232,700 zilitumika katika ujenzi, umaliziaji na ukarabati wa jumla ya maabara tisa (9) katika mikoa hiyo. Katika awamu ya pili iliyoanza kutekelezwa mwaka 2024/2025 kiasi cha Sh. Milioni 936.7 zimetumika kufadhili ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa vyumba vya maabara za sayansi vipatavyo 44 katika shule 20 za mikoa ya Songwe, Tabora na Kigoma.

Shule ya Sekondari ya wasichana Kakonko ni miongoni mwa shule zilizonufaika na ufadhili huo. Shule hiyo ya mchepuo wa sayansi ambayo ilipata wahitimu wa kidato cha nne kwa mara ya kwanza mwaka 2024, imebainisha manufaa yaliyotokana na ufadhili wa ujenzi wa maabara tatu za masomo ya Kemia, Biolojia na Fizikia.

Makamu Mkuu wa shule hiyo, Bw. Alex Lugaji Kagoma anasema, maabara hizo zimeleta mabadiliko makubwa kitaaluma. *“Wahitimu wetu wa kwanza 58 wa kidato cha nne wamefaulu kwa viwango vya juu; sita wamepata Daraja la Kwanza, 42 Daraja la Pili na tisa Daraja la Tatu. Hakuna aliyepata Daraja la Nne wala Sifuri,”.* Anaongeza kuwa, maabara hizo zimewawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo na kuwapa walimu nyenzo bora na rafiki za kufundishia.

Mafanikio hayo yanafanana na yale ya Shule ya Sekondari Itumba iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Ileje mkoani Songwe ambapo, ukamilishaji wa maabara mbili za sayansi umeongeza idadi ya wanafunzi wanaochagua mkondo wa sayansi.



Wanafunzi wakifanya mazoezi ya vitendo katika maabara ya Kemia ya Shule ya Sekondari Kamagi, Wilaya ya Sikonge, Mkoa wa Tabora.

...Inaendelea Uk.2

...Inatoka Uk.1

Bw. Deogratius Asigile Msusa Makamu Mkuu wa shule hiyo anaeleza kuwa, mwitikio wa wanafunzi wanaojiunga na masomo ya sayansi umeongezeka ikilinganishwa na kipindi cha nyuma ambapo shule ilikua haina maabara za sayansi.

Katika Shule ya Sekondari Nkangamo iliyopo Wilayani Momba mkoani Songwe, Mwalimu Mkuu wa Bw. Geofrey Mwakajila anasema, kabla ya ukarabati wa maabara tatu za sayansi, idadi ya wanafunzi waliokuwa wakijiunga na mchepuo wa masomo ya sayansi haikuzidi kumi, baada ya maboresho idadi ya wanafunzi wa mkondo wa sayansi imeongezeka.

Shule ya Sekondari Kamagi iliyopo Wilayani Sikonge mkoani Tabora ambayo pia ilinufaika na ufadhili wa ujenzi wa maabara za Biolojia na Kemia, wanafunzi wanachama wa Klabu ya STEM wameonesha ari mpya ya kujifunza kwenye miundombinu hiyo iliyoboreshwa.

Magreth Mayunga Mlolasa na Nadia Abubakar Mwingireza wanasema wamechagua masomo ya sayansi kwa kuwa yatawapa fursa ya kujiajiri na kutimiza ndoto zao za kitaaluma ambapo Magreth amepanga kuwa mfamasia na mjasiriamali wa kuuza dawa za binadamu.

Kassim Issa Mgayo mwalimu wa Kemia na Biolojia katika shule hiyo anathibitisha kuwa, uwepo wa maabara hizo umeongeza hamasa kwa wanafunzi wanaojiunga na shule hiyo kuchagua mkondo wa sayansi.

Shule nyingine za Sekondari zilizonufaika na miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya STEM ni pamoja na Shule ya Sekondari Kashoza (Kakonko), Gwanumpu (Kakonko), Migezi (Kibondo), Rugenge (Kakonko), Busami (Kibondo), Nyamidaho (Kasulu), Nyakitonto (Kasulu) Mount Samba (Kibondo) Masanga (Kigoma) zilizoko Mkoani Kigoma.

Katika mkoa wa Tabora shule nyigine zilizonufaika ni pamoja na Dkt. J.P. Magufuli (Kaliua), Goweka (Uyui), Langwa (sikonge), Ngulu (Sikonge), Kizengi (Uyui), Pangale (Sikonge) na Usagali (Uyui). Kwa upande wa Songwe shule za sekondari zilizonufaika ni Bupigu (Ileje), Shiwinga na Ndugu zote za Mbozi.

Kwa ujumla, miradi hii ya pamoja imelenga kuweka mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya STEM nchini, hatua inayochangia kuandaa kizazi chenye maarifa, ujuzi na ushindani katika dunia ya sasa ya sayansi na teknolojia.



Maabara za Sayansi katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kakonko, Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko, Mkoa wa Kigoma.

2. TEA YATOA REKODI: MIRADI 1,711 YATEKELEZWA THAMANI YA SH. BILIONI 128.5

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) imewasilisha mafanikio ya utekelezaji wa miradi mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, ikionyesha jinsi taasisi hiyo imekuwa chachu ya mabadiliko katika elimu nchini. Hatua hii inalenga kuboresha ufanisi katika usimamizi wa miradi inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na TEA.

Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Dkt. Erasmus Kipesha ametoa wasilisho hilo ikiwa ni sehemu ya mafunzo kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa lengo la kuwawezesha kuelewa vizuri majukumu na utendaji wa TEA na taasisi nyingine zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Katika kikao hicho, wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupatiwa ufafanuzi kuhusu jinsi TEA inavyosimamia na kuendesha Mfuko wa Elimu wa Taifa, ikiwemo miradi mbalimbali ya maendeleo ya shule kama vile mabweni, maabara, nyumba za walimu na vyoo.

Dkt. Kipesha alibainisha kuwa, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 hadi mwaka 2025/2026, jumla ya miradi 1,711 yenye thamani ya Sh. bilioni 128.5 imetekelezwa kupitia Mfuko wa Taifa wa Elimu ikionyesha mafanikio makubwa katika kuboresha miundombinu ya elimu na kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa watoto wa Kitanzania.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania akiwasilisha utekelezaji wa TEA mbele ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo

3. HABARI KATIKA PICHA








Maabara za Sayansi katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kakonko, Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko, Mkoa wa Kigoma.

4. HABARI KATIKA PICHA






Maabara za Sayansi katika Shule ya Sekondari ya Mtumba, Wilaya ya Ileje, Mkoa wa Songwe.




Wanafunzi wakifanya mazoezi ya vitendo katika maabara ya Kemia ya Shule ya Sekondari Kamagi, Wilaya ya Sikonge, Mkoa wa Tabora.



Baadhi ya wanafunzi wanaosoma masomo ya Sayansi kutoka Shule ya Sekondari Shiwinga iliyopo Wilayani Mbozi Mkoangi Songwe, wakifurahi mafunzo kwa vitendo katika maabara za kisasa zilizofanyika ukarabati na UNICEF kwa kushirikiana na TEA

5. MIRADI YA TEA MBULU YAINUA ELIMU KWA WATOTO KUTOKA MAZINGIRA MAGUMU

Miradi ya uboreshaji wa miundombinu ya shule Wilayani Mbulu mkoani Manyara imekuwa chachu ya mafanikio ya kitaaluma kwa wanafunzi wengi,hususan wale wanaotoka katika mazingira magumu.

Akizungumza Jijini Dodoma alipokutana na Mkurugenzi wa Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi Mhe. Zacharia P. Issaay Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini, alishukuru TEA kwa mchango wake mkubwa katika kuboresha maisha ya watoto walio katika mazingira magumu kielimu.

Mhe. Issaay aliambatana na Mhe. Emmanuel Nuwas Mbunge wa Mbulu Vijijini na lengo la ziara yao lilikuwa kutoa shukrani kwa ufadhili wa miradi iliyotekelezwa katika majimbo yao na kujadili mbinu bora za utekelezaji wa miradi zaidi siku zijazo. *“Miradi ya TEA imeinua hali ya elimu jimboni kwangu, hususan kwa watoto wa kike walio katika mazingira magumu,awali walikuwa wakitembea umbali mrefu kwenda na kurudi shuleni,”* alisema Mhe. Issaay.

Mbunge huyo aliongeza kuwa, katika Jimbo lake kuna zaidi ya miradi saba (7) iliyofadhiliwa na TEA ikihusisha ujenzi wa vyumba vya madarasa, mabweni ya wasichana, pamoja na nyumba za walimu, miradi inayolenga kuwezesha wanafunzi kupata elimu bora, salama na jumuishi.



Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini Mhe. Zacharia P. Issaay pamoja na Mbunge wa Mbulu Vijijini Mhe. Emmanuel Nuwas walipotembelea Ofisi za Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na kukutana na Mkurugenzi wa Utafutaji Rasilami na Usimamizi Miradi ya Elimu Bw. Masozi Nyirenda.

6. NMB BANK YAZIDISHA FURAHA SHULENI – WANAFUNZI WENYE ULEMAVU WAFURAHI

Benki ya NMB imepeleka tabasamu na matumaini katika shule tatu za msingi nchini baada ya kutoa vitimwendo (wheelchair) 30 kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, hatua inayowawezesha kushiriki kikamilifu katika masomo na kuboresha upatikanaji wa elimu jumuishi.

Mchango huo wenye thamani ya Sh.milioni 6.5, umetolewa kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kupitia Mpango wa Uwajibikaji wa Kijamii wa Makampuni (CSR) unaolenga kusaidia shule na wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Msaada huo umeelekezwa katika shule ya msingi ya Salvation Army Primary iliyopo Jijini Dar es Salaam, Shule ya Msingi Katumba II ya Jijini Mbeya na Shule ya Msingi Kilindoni ya kisiwani Mafia ambapo kila shule ilipata jumla ya 10.

Akizungumzia msaada huo Mkurugenzi wa Utafutaji Raslimali na Usimamizi Miradi ya Elimu Bw. Masozi Nyirenda amesema, mchango huo unaongeza upatikanaji wa elimu kwa usawa na kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu kuwa na mazingira wezeshi ya kujifunzia.

Mchango wa Benki ya NMB umeonesha jinsi taasisi za kifedha zinavyoweza kushirikiana na serikali na wadau wengine katika kuboresha elimu jumuishi nchini, huku wakitoa fursa sawa kwa kila mwanafunzi kujifunza katika mazingira bora na salama.

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Elimu Na. 8 ya mwaka 2001, imepewa jukumu la kuhamasisha michango na kuratibu shughuli za Uwajibikaji wa Kijamii wa Makampuni (CSR) kutoka kwa taasisi za umma, mashirika binafsi na wafadhili wanaojitolea.

Michango hiyo hutolewa kwa njia ya fedha, vifaa, au msaada wa aina nyingine na hutumika kwa ufanisi katika kutatua changamoto za mahitaji ya elimu, kwa kuzingatia ubora, usawa na upatikanaji wa elimu.



7. BWENI LA WASICHANA KICHEMA – SUMBAWANGA KUNUFAISHA WANAFUNZI 80



Bweni la wanafunzi wa kike katika Shule ya Sekondari Kichema Sumbawanga Mkoani Katavi

Bweni la wasichana katika Shule ya Sekondari Kichema, Manispaa ya Sumbawanga Mkoa wa Rukwa limekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wanafunzi. Bweni hilo lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80, limejengwa kwa fedha kutoka Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na TEA ambapo kiasi cha shilingi milioni 120 kimetumika.



Ujenzi wa bweni hilo umeboresha kwa kiasi kikubwa mazingira ya kujifunzia kwa kupunguza adha ya wanafunzi kutembea umbali mrefu kila siku. Hatua hiyo pia imeongeza usalama, muda wa kujisomea na kuimarisha ufaulu wa kitaaluma.

Meneja Miradi wa TEA, Mwafatuma Mohamed, ameipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kwa kusimamia vyema utekelezaji wa mradi huo na kuhakikisha bweni linakamilika na kuanza kutumika kama ilivyokusudiwa

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)

P.O. Box 2516, Ilazo - Dodoma.

info@tea.or.tz www.tea.or.tz officialteatz

"Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu Ya Elimu"